# MWISHO WA MUHULA WA KWANZA - 2020

*Muda: Saa 1 Dak. 40*

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Nilizaliwa na kulelewa__1__familia iliyotajirika. Baba yangu Pendawatoto__2__tajiri wa mali na moyo. Mimi na ndugu__3__hatukujua maana ya__4__kwani baba alitukidhia mahitaji yetu yote. Nyumbani__5__kila siku mlishiba na kutapika watu wa kila sampuli waliokuja__6__hali zao kwa baba. Baba aliwasaidia __7__mengi. Kuna waliopewa vibarua shambani na waliofanya kazi pale nyumbani. Almuradi kila mwana kijiji alifaidika kutokana na__8__wa baba. Ndugu yangu__9__aliishi __10__waja hawa na kuwaita waegemea nundu.


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. katika | B. kwa | C. ya | D. na |
| 2. | A. alipokuwa | B. alikuwa | C. alikua | D. aliweza |
| 3. | A. ndogo | B. dogo | C. mdogo | D. kidogo |
| 4. | A. kukosa | B. kuwepu | C. kupata | D. kulia |
| 5. | A. mwenu | B. petu | C. mwetu | D. mwao |
| 6. | A. kuomboleza | B. kulialia | C. kulia | D. kulilia |
| 7. | A. wa | B. cha | C. kwetu | D. kwa |
| 8. | A. mkono gamu | B. mkono wazi | C. mkono birika | D. mkono refu |
| 9. | A. kadogo | B. mdogo | C. kua | D. kwa |
| 10. | A. kuwatharau | B. kuwanusa | C. kuwapenda | D. kuwadharau |


Siku zilisonga na kupita__11__maji ya mto; hata nikajipata__12__shule ya msingi. Niliyakumbatia masomo yangu kwa hamu kubwa. Sikuwa na wakati wa kufanya__13__kwani baba hata na __14__lake kubwa hakuwahi__15__hisia za ugoigoi, nasi ilibidi tufuate nyayo zake.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. kama | B. ikiwa | C. iwapo | D. ingawa |
| 12. | A. katikati | B. katika | C. ndani | D. kati |
| 13. | A. chira | B. adili | C. ajizi | D. ajuza |
| 14. | A. mipato | B. kipato | C. pato | D. mapati |
| 15. | A. kudekezwa | B. kudekeza | C. kudedekezwa | D. kubarizi |

***Kutoka swali la 16 - 30 jibu kiulingana na maagizo.***

16. Taja maumbo haya mtawalia





A. kuru na kitovu  B. hori na duara
C. hori na kipenyo  D. kitovu an kuru

17. Mtoto wa paka huitwa kinyaunyau naye mtoto wa sungura ni
A. kidue  B. kitungul e
C. kisui  D. kiluwiluwi

18. Humusi ukizidisha na thuluthi ni_____
A. $^1/_{10}$  B. $^1/_8$
C. $^1/_{15}$  D. $^2/_{15}$

19. Kuku hukaa kizimbana nao mchwa hukaa
A. ghorofani B. mlimani
C. kichunguuni D. kichuguuni

20. Chagua sentensi iliyo katika hali tegemezi
A. Alikuja nikila
B. Mama alipika, akaosha vyombo kisha akapakua chakula
C. Bako alinipitia tuende shuleni
D. Ungekuja tungekula pamoja

21. Geuza kauli hii katika kauli halisi
**Mama alimwambia mwanawe aende dukani amnunulie maziwa**
A. "Kwenda dukani ukalete maziwa" mama alisema
B. "Nenda utanunua maziwa dukani," mama alimwambia mwanawe
C. Nenda uninunulie maziwa dukani," mama alimwambia mwanawe.
D. "Nenda uninunulie maziwa dukani," mama alimwambia mwanawe

22. Andika majina haya kwa ukubwa na udogo mtawalia: **Ndovu, mtoto na kichwa**

| | |
|---|---|
| A. dovu kidovu<br>mtoto - matoto<br>kichwa - jichwa | B. Dovu - kidovu<br>Toto - kitoto<br>jichwa - kijichwa |
| C. kidovu - dovu<br>kitoto - toto<br>kijichwa - jichwa | D. ndovu - kidovu<br>mtoto - kitoto<br>kichwa - kijichwa |

23. Sentensi hii hupatikana katika ngeli gani?
**Kusoma huku ndiko kutakakufaa**
A. U - U B. KU - KU
C. LI - YA D. YA - YA

24. Andika sentensi hii upya bila **'amba'**
Nyama ambazo zilozoliwa zilioza
A. Nyama zilizoliwa zilioza
B. Nyama ambazo zilizoliwa zilioza
C. Nyama zilizolia zilioza
D. Nyama zilizokuliwa zilioza

25. Chagua sentensi iliyo na ndi-kisisitizi
A. Ndio nimo darasani
B. Mimi ndimi mwalimu wa kiswahili
C. Viatu hivyo ndivyo vyako
D. Ninyi ni wanafunzi

26. Tumia kivumishi kisisitizi kukamilisha sentensi hii
**Kijana_____ni bingwa wa kadanda.**
A. uyu huyu B. wawa hawa
C. yuyu huyu D. huyu huyu

27. Mbuzi ni mnyama afugwaye nyumbani. Mbuzi pia ni_______
A. jina la matusi
B. mnyama aishiye mbugani
C. kifaa kinachotumiwa kukunia nazi
D. kifaa cha kupikia

28. Kati ya nyuni hawa, ni kundi lipi la nyuni wanaofugwa nyumbani?
A. Njiwa, kuku, mwewe na tai
B. Mwewe, tai, bundi na batamzinga
C. Mwewe, tai, bundi na heroe
D. Kuku, batamzinga na mtetea

29. Mtoto wa mwana ni mjukuuu. Je, mtoto wa mjukuu ni nani?
A. Mjukuu B. Kilembwe
C. Kilebwekeza D. Kitukuu

30. Tumia -o-ote, kukamilisha sentensi hii
**Njia _____zinapaswa kutumiwa vizuri**
A. yoyote B. lolote
C. wowote D. zozote

***<u>Soma shairi hili kisha ujibu maswali</u>***
***<u>31 mpaka 40.</u>***

Wakenya sikilizeni, vijana twawambieni,
Tunaamini upendo, kwa sisi sote nchini,
Karibia siwe kando, toka bara hadi pwani,
Kutengana ni uvundo, jamani tupendaneni.

Wakenya sikilizeni, tunaamini amani,
Tutulie tulituli, wote tuwe furahini,
Tukila sima na wali, sote tukiwa watani,
Neema kila mahali, itasambaa jamani.

Wakenya sikilizeni, tunaamini elimu,
Twatala kusoma sana, mepesi pia magumu,
Yote hayo ya maana, msife moyo walimu,
Tutajua yanofana, wetu utu utadumu.

Sikilizeni wakenya, twawaamini wazee,
Na vijana twawamini, kila mtu wa pekee,
Mwenye kilema, mwilini wazima na wamlee
Afurahi maishani, tabu tumpunguze.

31. Shairi hili ni la beti ngapi?
A. Sita.
B. Saba.
C. Nne.
D. Tatu.

32. Maneno ya kurudiwarudiwa yako kwenye mshororo upi?
A. Wa mwisho
B. Unaotangulia
C. Wa pili
D. Haijulikani

33. Mishororo imegawanyika katika sehemu ngapi ngapi?
A. mbili mbili
B. Nne nne
C. nane nane
D. tatu tatu

34. Kina cha kati katika ubeti wa mwisho ni -ni- na cha nje katika ubeti huo huo ni e, vina vya ubeti wa kwanza ni vipi?
A. do, na ni
B. ni na ni
C. ndo na ni
D. na na imu

35. Shairi la majibizano linajulikana kama
A. ngojera
B. unne
C. tarbia
D. tathlitha

36. Shairi hili ni la aina ya____________
A. tarbia
B. takmisa
C. tathnia
D. tathlitha

37. Kuna mizani ngapi kwenye kila sehemu?
A. nane nane
B. nne nne
C. mbili mbili
D. kumi kumi

38. Ni kina nani wasimulizi wa shairi hili?
A. Wakenya
B. Wazee
C. Vijana
D. Raia

39. **"Tutulie tulituli"** ni msemo. Je, <u>kutengana ni uvundo</u> ni nini?
A. Kitendawili
B. Msemo
C. Ufananisho
D. Methali

40. Elimu ina matokeo gani ya kudumu?
A. Tabia njema ya siku zote.
B. Neema ya kila mahali.
C. Furaha maishani.
D. Watu kupendana.

***<u>Soma habari hiio kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>***

Dunia inasonga mbele kwa sababu ya mawasiliano. Watu wanapowasiliana hufanya biashara ya kuendeleza uchumi na pia kubadilishana mawazo. Mawasiliano ni uwezo wa kufikisha watu, vitu, mawazo, maoni, au habari kutoka pahali pamoja hadi pengine.

Kuna njia nyingi za kuwasiliana. Njia moja ni matumizi ya vyombo na vifaa vya usafirishaji katika nchi kavu, majina na angani. Kunazo mashine kama redio, televisheni,simu,faksi na mitambo mingine ya kompyuta. Zaidi ya hayo, kunayo mawasiliano ya barua, telegramu, vitabu au magazeti.

Kuhusu uandishi wa barua za magazetini mtu yeyote anaweza kuwasilisha maoni yake.

Mwasilishaji huyo anaweza kuwa mume au mke, raia au mtawala, msomi au asiye na kisomo, mzee au kijana - hata kijana wa shule ya msingi. Kenya ni mojawapo wa nchi chache dunia ni zilizo na uhuru wa habari na kujieleza.

Msomaji yeyote akiwa na jambo la kweli, la maana, lenye umuhimu kwake na kwa watu wengine, ana haki na wajibu wa kuliwasilisha kwenye vyombo vya mawasiliano. Siku hizi uvumbuzi wa tarakilishi, televisheni na rununu zimefanya mawasiliano kuwa rahisi sana. Ukiwa Kenya au nchi nyingine ya Afrika unaweza kuwasiliana na mtu aliye ng'ambo kwa kuitumia tarakilishi, faksi au simu. Mawasiliano yameleta ufanisi mwingi duniani.

41. Ni nini kinachosukuma dunia mbele?
   A. Mzunguko wa jua
   B. Mawasiliano
   C. Masomo
   D. Umaskini

42. Kulingana na habari hii, kuna biashara gani kwenye mawasiliano?
   A. Kubadilishana mawazo na kuendeleza uchumi
   B. Kunufaisha mtu binafsi.
   C. Kutojenga taifa.
   D. Kutoendeleza uchumi

43. Simu ya mkono pia inajulikana kama
   A. faksi
   B. barua pepe
   C. tarakilishi
   D. rununu

44. Kutokana na habari hii, ni zipi sio njia za kisasa za mawasiliano?
   A. piga mbuzi, ngoma na uvuko wa moshi
   B. Redio, barua pepe na rununu
   C. Telegramu, redio na simu
   D. Faksi, radio na tarakilishi

45. Chagua aina ya mawasiliano yenye maandishi
   A. Vitabu, magazeti na redio
   B. Tarakilishi, rununu na magazeti
   C. Vitabu, magazeti na barua
   D. Redio pekee

46. Kulingana na habari hii, ni nini huchangia barua kuchapishwa na mhariri?
   A. Uwepo wa anwani ya barua
   B. Hati nadhifu
   C. Anwani, majina kamili na sahihi
   D. Majina kamili na sahihi

47. Mwandishi anasisitiza kwamba
   A. Jambo la maana na ukweli haliwezi kuchapishwa
   B. Mawasiliano hutegemea kifaa ambacho kimevumbuliwa
   C. Mwandishi mwenye hati nadhifu ndiye tu anayeweza kuwasilisha mawazo yake
   D. Jambo la maana na la kweli kwa watu wengine huweza kuchapishwa

48. Kauli ***"...ana haki na wajibu wa kuliwasilisha kwenye vyombo vya mawasiliano"*** ni mojawapo ya haki za Wakenya. Haki hii hupatikana wapi?
   A. Kwenye radio
   B. Kwenye katiba ya Kenya
   C. Kwenye Bunge
   D. Shuleni

49. Maneno mume na mke kwa jumla ni
   A. maumbile
   B. jinsia
   C. binadamu
   D. raia

50. Kichwa mwafaka kwa habari hii ni
   A. Mawasiliano
   B. Uchukuzi
   C. Haki
   D.Redio